



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA ZA WATENDAJI WA  
VITUO VYA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA  
WAPIGA KURA

Kwa madhumuni ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7 (4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 Mkurugenzi wa Uchaguzi anakaribisha maombi kutoka kwa watazania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za waandishi wasaidizi na waendeshaaji wa vifaa vya bayometriki.

**A. SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA MWANDISHI MSAIDIZI**

- (a) awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au zaidi na anajua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
- (c) awe mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta au simu janja (Smartphone);
- (d) awe ni mkazi wa mtaa au kijiji katika kata anayoomba kuwa mwandishi msaidizi;
- (e) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa; na
- (f) awe ni mwadilifu na mtiifu.

**B. SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA MWENDESHAJI WA VIFAA VYA BAYOMETRIKI**

- (a) awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au zaidi na anajua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
- (c) awe mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta au simu janja (Smartphone);
- (d) awe ni mkazi wa mtaa au kijiji katika kata anayoomba kuwa mwendeshaaji wa kifaa cha bayometriki;
- (e) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa; na
- (f) awe ni mwadilifu na mtiifu.

### C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo:-

- i. Kwa siku za uboreshaji wa Daftari vituoni waandishi wasaidizi na waendeshaji wa vifaa vya bayometriki watalipwa posho ya Shilingi 50,000/= kwa siku na nauli Shilingi 10,000/=.
- ii. Wakati wa mafunzo, waandishi wasaidizi na waendeshaji wa vifaa vya bayometriki watalipwa posho ya Shilingi 50,000/= na nauli Shilingi 10,000/= kwa kila siku ya mafunzo.

### D. MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji lazima aainishe nafasi anayoomba pamoja na kata anayoomba kufanyia kazi.
- ii. Mwombaji aambatishe:-
  - a. nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na Taaluma vinavyohitajika kulingana na kada husika kama vilivyofafanuliwa katika Tangazo hili.
  - b. wasifu (CV) ukionesha anuani yake ya makazi, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini wake wawili.
  - c. picha mbili zenye ukubwa sawa na picha iliyomo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.
  - d. barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa serikali ya mtaa au kijiji katika eneo analoishi.
- iii. Mwombaji ambaye ni mtumishi wa umma apitishie barua yake ya maombi kwa mwajiri wake.

**MWOMBAJI ATAKAYEBAINIKA KUWASILISHA TAARIFA ZA KUGHUSHI ATACHUKULIWA HATUA ZA KISHERIA.**



Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo: -


Mkurugenzi wa Uchaguzi,  
Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,  
Uchaguzi House,  
Enco la Uwekezaji Njedengwa,  
Kitalu D, Kiwanja Na.4,  
5 Barabara ya Uchaguzi,  
S.L.P. 358,

41107 DODOMA.

ILI KURAHISISHA UTUMAJI WA MAOMBI, BARUA ZOTE ZIKIWA  
ZIMEFUNGWA ZIPELEKWE KWA MTENDAJI WA KATA AMBAYE  
ATAZIPOKEA NA KUZIWASILISHA KWA MKURUGENZI WA  
HALMASHAURI

MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI NI TAREHE 27 APRILI, 2024

Limetolewa na:

  
Kailima, R.K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI  
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI  
DODOMA.

15 APRILI, 2024

